



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



WIZARA YA AFYA

MAMLAKA YA DAWA NA VIFAA TIBA

TAARIFA YA UKAGUZI WA DAWA, VIFAA TIBA NA VITENDANISHI KATIKA KIPINDI CHA

2021/2022

KANDA YA MASHARIKI

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba, TMDA Kanda ya Mashariki
P. O. Box 31356, Jengo la Victoria House, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi, Dar es Salaam
Tel: +255-737-226328/788470301, Fax: +255-22-2450793
Website: www.tmda.go.tz, Email: info.eastzone@tmda.go.tz

1.0. Utangulizi

Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) inajukumu la kulinda afya ya jamii kwa kudhibiti ubora, usalama na ufanisi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi. Taarifa hii inaonesha utekelezaji wa kazi ya ukaguzi kwa Ofisi ya Kanda ya Mashariki katika kipindi cha kuanzia Julai 01,2021 hadi mwaka Juni 30, 2022 ambazo ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa miaka mitano wa Mamlaka. Pia Kanda ya Mashariki inashiriki operesheni maalumu ambazo huwa zinafanyika nchi nzima kila inapopangwa na kutoa elimu kwa jamii juu ya athari za matumizi ya bidhaa za tumbaku na katazo la kuzuia uvutaji wa sigara katika mikusanyiko ya watu.

2.0 Lengo la ukaguzi

Ukaguzi ulilenga kufuatilia ubora wa dawa za binadamu na mifugo, vifaa tiba na vitendanishi vinavyosambazwa au kuuzwa katika maduka, maghala, na vituo vya afya, zahanati na hospitali za serikali na binafsi kwa kuhakiki utekelezaji wa Sheria kwa :

- 2.1 Kubaini uwepo wa dawa, chanjo, vifaa tiba na vitendanishi ambavyo havijasajiliwa
- 2.2 Kubaini uwepo wa dawa, chanjo, vifaa tiba au vitendanishi duni sokoni
- 2.3 Kubaini uwepo wa dawa bandia sokoni
- 2.4 Kubaini uwepo wa bidhaa zilizokwisha muda wa matumizi
- 2.5 Kuhakiki ubora wa majengo, mifumo ya utengenezaji, na mazingira ya uzalishaji, usambazaji, uhifadhi na uuzaaji.
- 2.6 Kutoa elimu kwa jamii juu ya athari za matumizi ya bidhaa za tumbaku na katazo la kuzuia uvutaji wa sigara katika mikusanyiko ya watu.

3.0 Ukaguzi wa maeneo ya kutengenezea na kuuzia bidhaa

Katika kipindi cha kuanzia **Julai 01, 2021** hadi **June 30, 2022** Kanda ya Mashariki ilikagua jumla ya maeneo **2,274** yalikaguliwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Tanga ambapo famasi za dawa za binadamu **521**, maghala ya dawa **163**, viwanda **31**, maduka ya dawa za mifugo **356**, DLDM **806**, hospitali **78**, kliniki za kibingwa (*polyclinics*) **40**, zahanati **133**, maabara **51**, maduka ya vifaa tiba **57**, maghala ya vifaa tiba **24** na maduka ya kawaida (*general sales*) **14**.

Hatua mbalimbali zilichukuliwa kwa maeneo ambayo hayakukidhi matakwa ya Sheria ikiwa ni pamoja na kuondoa bidhaa duni na ambazo hazijasajiliwa, kutoa muda wa kufanya marekebisho ya majengo

yaliyokuwa na mapungufu, kuondoa dawa duni, kulipia 25% ya gharama ya dawa zilizoondolewa sokoni kama gharama ya kuziteketeza. Mchanganuo wa majengo yote yaliyokaguliwa umeainishwa katika jedwali hapo chini:

Jedwali: Ukaguzi wa maeneo ya biashara ya dawa na vifaa tiba

Mkoa	Famasi	Maghala (Dawa za binadamu) Viwanda	Maduka ya dawa za mifugo DLDM (Dawa za binadamu)	Hospitali	Kliniki za kibingwa polyclinics	Zahanati	Maabara	Maduka ya Vifaa Tiba	Maghala (Vifaa Tiba)	Maduka ya kawaida	Jumla		
Dar es Salaam	429	161	25	220	469	54	32	46	45	54	18	14	1,567
Tanga	28	-	-	106	189	11	-	39	-	-	-	-	373
Pwani	64	2	6	30	148	13	8	48	6	3	6	-	334
Jumla	521	163	31	356	806	78	40	133	51	57	24	14	2,274

4.0 Uteketezaji wa bidhaa zisizokidhi viwango

Jumla ya tani 394.39 za bidhaa zisizokidhi viwango zenyé thamani ya TZS: 8,944,671,898.40/= ziliteketezwa. Mchanganuo wa bidhaa husika ni kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapo chini:

Jedwali : Uteketezaji wa bidhaa zisizokidhi viwango

Na.	Aina ya bidhaa	Mchanganuo			
		Vilivyotolewa taarifa kwa hiari		Vilivyokamatwa	
		Uzito (MT)	Thamani (TZS)	Uzito (MT)	Thamani
1.	Dawa	261.39	6,848,629,888/=	00	00
2.	Vifaa tiba+ Vitendanishi	133	2,096,042,010.40/=	00	00
	Jumla	394.39	8,944,671,898.40/=	00	00

5.0 CHANGAMOTO

Changamoto zilizojitokeza ni pamoja na:

- 5.1 Uingizaji wa bidhaa nchini kidogokidogo kupitia njia zisizo rasmi hasa kutoka nchi za jirani na Tanzania kwa kutumia usafiri ikiwemo bodaboda na baiskeli.
- 5.2 Kuingiza nchini bidhaa ambazo hazijasajiliwa/bandia kwa kuficha bidhaa ndani ya mabegi ya nguo na kusafirisha kwenye mabasi kupitia vituo rasmi vya forodha.
- 5.3 Pamoja na kaguzi zinazofanywa na TMDA Kanda ya Mashariki kila siku bado kuna baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu wanaofanya biashara za dawa bila kuzingatia taratibu na sheria zilizowekwa.

6.0 MAFANIKIO

Kuongezeka kwa utii bila shuruti (*voluntary compliance*) kwa wafanyabiashara wa bidhaa tunazozidhibiti. Hii imedhihirika kwa mfano wateja kutoa taarifa bidhaa zinapokuwa zimeisha muda wa matumizi ili ziteketezwe.

7.0 HITIMISHO

TMDA Kanda ya Mashariki inatoa shukrani za dhati kwa wadau mbalimbali pamoja na uongozi wa TAMISEMI na wadau wengine kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakitupatia katika kuhakikisha kuwa tunatekeleza kazi za ukaguzi.

IMEANDALIWA NA TMDA KANDA YA MASHARIKI



A. A. BITEGEKO

MENEJA WA KANDA